Pokea ana kwa ana msaada wa kukamilisha maombi haya katika maeneo yafuatayo:

Kituo cha Matibabu cha Dartmouth-Hitchcock
(Dartmouth-Hitchcock Medical Center)
Huduma za Kifedha za Mgonjwa/Jengo Kuu
Lenye Maduka (Patient Financial Services/
Main Mall)
One Medical Center Drive
Lebanon, NH 03756

Dartmouth-Hitchcock Concord
Mshauri wa Fedha/Ghorofa ya 1
(Financial Counselor/Level 1)
253 Pleasant Street
Concord, NH 03301

Dartmouth-Hitchcock Manchester
Washauri wa Fedha/Mashariki & Magharibi
Ghorofa ya 1 (Financial Counselors/
East & West Level 1)
100 Hitchcock Way
Manchester, NH 03104

Dartmouth-Hitchcock Nashua
Mshauri wa Fedha/Ghorofa ya 1
(Financial Counselor/Level 1)
2300 Southwood Drive
Nashua, NH 03063

Alice Peck Day Memorial Hospital
Mshauri wa Usajili/Fedha (Registration/
Financial Counselor)
10 Alice Peck Day Drive
Lebanon, NH 03766

Cheshire Medical Center
Ukumbi Mkuu wa Usajili/Makeshia
(Registration/Cashiers Main Lobby)
580 Court Street
Keene, NH 03431

New London Hospital
Washauri wa Fedha/Mapokezi
(Financial Counselors/Reception)
273 County Road
New London, NH 03257

Mpigie simu moja ya Mawakili wetu wa Wagonjwa kwa:

(844) 647-6436.

Tafadhali tuma maombi yaliyokamilika kwa:

Dartmouth-Hitchcock
Attn: PFS - Level 3 – FAA
One Medical Center Drive
Lebanon, NH 03756-0001

Alice Peck Day Memorial Hospital
Attn: PFS
10 Alice Peck Day Drive
Lebanon, NH 03766

Cheshire Medical Center
Attn: PFS – FAA
580 Court Street
Keene, NH 03431

New London Hospital
Attn: Financial Counselor
273 County Road
New London, NH 03257

Dartmouth-Hitchcock Health

dartmouth-hitchcock.org/assistance

Sera ya Msaada wa Kifedha

Dartmouth-Hitchcock Health

Je, unahijati msaada wa kulipia bili yako kwa huduma za dharura au zenye umuhimu kimatibabu kwa Hospitali za Dartmouth-Hitchcock, Alice Peck Day Memorial Hospital, Cheshire Medical Center au New London Hospital?

Unaweza kuwa unastahili kupata msaada wa kifedha.

Dartmouth-Hitchcock, Alice Peck Day Memorial Hospital, Cheshire Medical Center na New London Hospital zinatoa huduma za hisani za bure au zenye punguzo kwa huduma za dharura au zenye umuhimu wa kimatibabu zinazotolewa kwa wagonjwa watakaofuzu. Wagonjwa ambao wataonekana wanastahili kupata msaada wa kifedha huenda wasitozwe zaidi ya huduma inayotozwa kwa wagonjwa wenye bima kwa huduma za dharura au zenye umuhimu kimatibabu kwa huduma sawa.

Sera ya Fedha ya D-HH

Dartmouth-Hitchcock, Alice Peck Day Memorial Hospital, Cheshire Medical Center na New London Hospital zitatoa huduma kwa hali za dharura za kimatibabu na huduma muhimu za kimatibabu kwa watu bila kujali uwezo wao wa kulipia au ustahili wa msaada wa kifedha au serikali na bila kujali umri, mbari, rangi, hali ya kijamii au uhamiaji, mwelekeo wa kingono au dini. Tunatoa msaada wa kifedha kwa watu ambao (i) ni wakazi wa New Hampshire au Vermont, au wasio wakazi ambao watapata dharura ya kimatibabu wakati wako maeneo haya; wasio na bima au walio na bima ya afya lakini wanahitaji msaada wa kifedha kuwasaidia kufadhili gharama za nje ya mfukoni kama makato, malipo ya pamoja na bima ya pamoja; hawastahili kwa programu yoyote ya kiserikali ya manufaa ya huduma za afya; na wanatimiza vigezo vya ustahili wa msaada wa kifedha kama inavyoelezwa kwenye Sera yetu ya Msaada wa Kifedha. Hali za mahali husika au utenganifu vinaweza kutumiwa kama inavyoelezwa zaidi kwenye Sera yetu ya Msaada wa Kifedha. Wagonjwa wanatarajiwa kufuata taratibu kwa kupata msaada wa kifedha au aina nyingine ya malipo na kuchangia kwenye gharama za huduma zao kulingana na uwezo wao binafsi wa kulipa. Watu wanaoweza kununua bima ya afya wanategemewa kufanya hivyo, ili kuhakikisha kufikia huduma za kiafya ambazo zinanufaisha afya zao kwa ujumla pamoja na kuwapa ulinzi wa mali zao binafsi.

Jinsi gani na ni muda gani wa kufanya maombi ya msaada wa kifedha?

Unaweza kufanya maombi muda wowote wakati wa kupokea huduma yako au katika mzunguko unaofuata wa ukusanyaji. Hata hivyo, tunasisitiza sana maombi yakamilishwe kabla ya miadi. Mawakili wa Wagonjwa wanaweza kukusaidia kutambua na kuomba ufadhili wa bima au vyanzo vingine na kwa kukamilisha maombi kwa ajili ya msaada wa kifedha. Ikiwa una salio lililobaki baada ya kumaliza vyanzo vingine vyote vya ufadhili, unaweza kustahili kupata msaada wa kifedha. Maombi yanaweza kufanywa na mtu mwenyewe, kwa njia ya simu, au kupatikana kupitia kiungo kilicho hapa chini.

Kiasi cha punguzo

Ikiwa haustahili kupata msaada wa kifedha, bado unaweza kustahili kupata punguzo lisilo la bima au mapunguzo mengine kulingana na Sera yetu. Punguzo hili lisilo la bima linatumiwa kabla ya kumpa mgonjwa bili na kabla ya kutumia marekebisho yoyote ya msaada wa kifedha. Punguzo linatokana na njia ya “uchunguzi wa Mpango wa Huduma za Afya” kama inavyoelezwa chini ya kanuni zinazotumika ikitekeleza Sehemu ya 501(r) ya Kanuni za Mapato ya Ndani. Kiasi cha punguzo kinaweza kutofautiana kulingana na kituo.

Msaada wa Kifedha unakadiriwa vipi?

Kiasi cha msaada wa kifedha unachokipokea kinategemeana na jumla kuu ya kipato na mali kulingana na miongozo ya serikali ya umaskini.. Unaweza kufuzu: Ikiwa kipato cha familia yako kiko kwa au chini ya 300% ya Kima cha Serikali cha Umaskini; unaotolewa na Marekani. Idara ya Afya na Huduma za Binadamu (HHS) na inayosasishwa kwa kila mwaka; au ikiwa unaamini kwamba mali zako, mali za ukwasi na rasilimali zingine zinazopatikana havitoshi kulipia gharama ya huduma yako. Kwa kuongezea kwa maombi yako yaliyokamilika, tunaweza kuhitaji nyaraka zinazothibitisha kipato chako, mali na gharama za matibabu kutathmini iwapo unafuzu kupata msaada wa kifedha. Utataarifiwa ndani ya siku 30 baada ya kupokea maombi yako na taarifa zote za muhimu iwe maombi yamekubaliwa au yamekataliwa chini ya sera yetu. Kwa ombi lako, fomu ya maombi ya fedha au nakala ya Sera ya Msaada wa Kifedha vitatumwa kwako bila malipo. Pia, nyaraka hizi na muhtasari huu vinapatikana katika tovuti yetu ya dartmouth-hitchcock.org/billing-charges/financial_assistance.html or cheshire-med.com/patients_visitors/financial_assistance.html.

Nyaraka hizi pia zinapatikana katika lugha zifuatazo: Kihispania, Kifaransa, Kireno, Kichina, Kigiriki, Kivietnamu, Kinepali, Kiarabu na Kirusi.